



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOMBA



Unapojuji tafadhalii taja:

Kumb. Na. MODC/ A10/38VOLII/57

21 Mei, 2024

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba alipokea kibali cha Ajira kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa barua yenye Kumb. Na. FA.228/613/01/B/015 ya tarehe 22 Aprili, 2024. Hivyo anawatangazia Watanzania wote wenye sifa kutuma maombi kwa nafasi zifuatazo;

1.0 MWANDISHI MWENDESHA OFISI DARAJA LA II - NAFASI 1

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

- Mwombaji awe na Cheli cha Kidato cha Nne (Form IV) na mwenye Stashahada (Diploma) ya Uhazili au cheti cha NTA level 6 ya Uhazili.
- Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na kupata programu ya kompyuta za ofisi kama vile: word, Excel, powerpoint, Internet, E-mail na Publisher kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

1.2 KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida na siri.
- ii. Kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- iii. Kutunza taarifa na kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine.
- iv. Kutafuta majalada na nyaraka zinazohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya kazi.
- v. Kupokea majalada na kusambaza kwa Maofisa walio katika Idara/Kitengo/Sehemu husika.
- vi. Kukusanya, kutunza na kuyarejesha majalada na nyaraka sehemu zinazohusika.
- vii. Kupanga dondo na kufanya maandalizi ya vikao mbalimbali na
- viii. Kuandaa orodha ya mahitaji vya vifaa vya ofisi.

1.3 MSHAHARA

- Mshahara atalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali TGS C1

2.0 MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenyе umri kuanzia miaka 18 na wasiozidi miaka 45.
- ii. Waombaji wenyе ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa kuombea ajira aina ya ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza Curriculum Vitae (CV) yenyе Anuani inayotumika, namba ya simu na anuani ya Barua Pepe (E-mail address) pamoja na majina ya Wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Matokeo ya muda (provisional/Testimonials/ Statement of Results) havitakubaliwa.
- v. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.
- vi. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- vii. Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na warnejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi ya kazi kwa waajiri wao na waajiri wao wajiridhishe ipasavyo.
- viii. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba 2010.
- ix. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne, Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia zifa za kazi husika.
- x. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimethibitishwa na Mamlaka husika (TCU, NACTEVET na NECTA).
- xi. Uwasilishaji wa Taarifa na Sifa za kughushi, watusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- xii. Barua ya maombi itatakiwa iandikwe kwa Kiswahili au Kingereza.
- xiii. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 03 Juni, 2024.
- xiv. MUHIMU: kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya Elimu, aidha anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:

Mkurugenzi Mtendaji,


Halmashauri ya Wilaya ya Mombasa,

S.L.P 273,

MOMBASA.

- xv. Maombi yote ya kazi yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo: <https://portal.ajira.go.tz/advert/index> anuani hii pia inapatikana kwenye Tovuti ya Sekterarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa "Recruitment Portal".
- xvi. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.

Imetolewa na;


Alex S. Batwe
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOMBA

